

# UGONJWA WA VIKOPE.

## UGONJWA WA VIKOPE.



### Ugonjwa wa vikope ni nini?

Ugonjwa wa vikope, ni hali ambayo kope hujikunjia kwa ndani kuelekea kwenye jicho na hivyo husugua katika kioo cha mbele cha jicho. Kope zote au chache zinaweza kujikunjia ndani ya jicho na kukugusa katika kioo cha mbelel cha jicho. Mtu mwenye ugonjwa wa vikope husikia maumivu ya jicho au kama macho yana mchanga.

**Wahi sasa kutibiwa usichelewe!**

Wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo;

Kilimanjaro Centre For  
Community Ophthalmology,

P.O.Box 2254,

Moshi,

Tanzania.

Phone: 255 27 275 3547

Fax: 255 27 275 3598

Email: [kcco@kcmc.ac.tz](mailto:kcco@kcmc.ac.tz)



### ◆ Ugonjwa wa vikope husababishwa na nini?

Kuna sababu nyingi, lakini mara nyingi ni makovu yaliyopo katika kifuniko cha jicho kwa sababu ya maambukizo y a maramara na ugonjwa wa trakoma. Sababu nyingine za ugonjwa wa vikope ni kuungua, jeraha katika kifuniko cha jicho, au ukoma.

### ◆ Madhara ya ugonjwa wa vikope ni yapi?

Kama kope zikiendelea kusugua kwenye kioo cha mbele cha jicho kwa muda mrefu, husababisha makovu katika kioo. Kioo cha mbele cha jicho(konea) ni dirisha lililo wazi mbele ya jicho. Kama kioo cha mbele cha jicho kikipata kovu dirisha haliwezi kuwa wazi na jicho haliwezi kuona tena.

### ◆ Je kila mtu mwenye ugonjwa wa vikope anaweza kuwa kipofu?

Hapana. Upofu unaweza kutokea wakati kope zinaposugua katika kioo cha mbele cha jicho. Wakati mwingine, kope chache zinaweza kusababisha uharibifu wa kioo cha mbele cha jicho. Ukiweza kusawazisha kope zilizojikunjia ndani ya jicho, kwa upasuaji mdogo (kama ilivyoelezwa hapo chini) kabla uwezo wa kuona haujahiribika, upofu unaweza kuzuilika.

### ◆ Je ni nani anayeweza kupatwa na ugonjwa wa vikope?

Ugonjwa wa vikope unaweza kuwapata watu wa liko zote, ingawa hali hii mara nyingi huwapata watu wazima. Wanawake huathirika na ugonjwa wa vikope zaidi kuliko wanaume.

### ◆ Je unaweza ukatibuje ugonjwa wa vikope?

Njia sahihi ni kufanyiwa upasuaji mdogo, unaoitwa “kusawazisha kope”. Upasuaji unaweza kufanywa katika kliniki ndogo/zahanati au katika kituo cha afya au katika darasa la shule na muuguzi au afisa tabibu msaidizi aliyepata mafunzo. Upasuaji huu hufanywa kwa kuchanwa kidogo katika kifuniko cha jicho na kisha kushona kwa nyuzi. Na mwisho wa upasuaji kope huzungushwa na kuelekezwa nje ya mboni ya jicho na kurudia katika hali ya kawaida.

Mara nyingi baadhia ya nyuzi huachwa kwa wiki moja, na baadaye kuondolewa. Ni hali ya kawaida baada ya upasuaji kifuniko cha jicho huwa na kidonda na wekundu kwa siku chache, lakini baada ya wiki chache jicho hurudia katika hali ya kawaida.

### ◆ Je unaweza kutatua tatizo la ugonjwa wa vikope kwa kunyofoa kope mwenyewe?

Kope zinazogusa au kusugua katika kioo cha mbele cha jicho zinaweza kuondolewa/kunyofolewa kwa kutumia “fosepsi”, ingawa zinaweza kuota tena na kuanza kusugua tena katika kioo cha jicho. Mbali na hayo, kama zikinyofolewa kope zinazobaki huwa na ncha kali sana na ni rahisi kuharibu jicho. Kunyofoa kope siyo njia sahihi ya kutatua tatizo la ugonjwa wa vikope. Kusawazisha kope ndiyo njia sahihi.

### ◆ Je ugonjwa wa vikope unaeza kurudia baada ya kusawazishwa kope?

Ndiyo, wakati mwingine unaweza kurudia, kwa sababu ya uharibifu wa muda mrefu wa kifuniko cha jicho. Kuna mambo machache ambayo yanaweza kufanyika ili kuzuia ugonjwa wa vikope usiweze kurudia. Kama ukirudia unaweza kufanyiwa upasuaji mdogo (kusawazishwa kope) tena.

